

KUMB: PPR/18 - 06/1

TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI KIKOMO ZA MAFUTA AINA YA PETROLI KUENZIA JUMATANO, TAREHE 6 JUNI 2018

Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), inatangaza bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli hapa nchini. Bei hizi zitaanza kutumika kuanzia **Jumatano, Tarehe 6 Juni 2018**. Pamoja na kutambua bei kikomo za bidhaa mbalimbali za petroli nchini, ni muhimu kuzingatia yafuatayo:-

- (a) Bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya aina zote (Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa) yaliyoingizwa nchini kupitia bandari ya Dar es Salaam, zimebadilika ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 2 Mei 2018. Kwa mwezi Juni 2018, bei za rejareja za Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimeongezeka kwa Shilingi 55/lita (sawa na asilimia 2.47), Shilingi 19/lita (sawa na asilimia 0.88) na Shilingi 36/lita (sawa na asilimia 1.68), sawia. Vilevile, ukilinganisha na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa nazo zimeongezeka kama ifuatavyo; Shilingi 54.85/lita (sawa na asilimia 2.61), Shilingi 18.83/lita (sawa na asilimia 0.93) na Shilingi 36.08/lita (sawa na asilimia 1.78) sawia. Kwa kiasi kikubwa, mabadiliko ya bei za mafuta ya Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa kwenye soko la ndani yametokana na kuongezeka kwa bei za mafuta hayo katika soko la dunia , ongezeko la gharama za usafirishaji wa mafuta hayo (*BPS Premiums*), ongezeko la gharama linalotokana na meli kuchelewa kushusha shehena ya mafuta bandarini (*demurrage charges*) na kushuka kwa thamani ya Shilingi ya Tanzania dhidi ya dola ya Marekani, fedha inayotumika kununua mafuta.
- (b) Bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya Petroli na Dizeli yaliyoingizwa nchini kupitia bandari ya Tanga zimebadilika ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 2 Mei 2018. Katika toleo hili la Juni 2018, bei za rejareja za Petroli na Dizeli kwa Mikoa ya Kaskazini zimeongezeka kwa Shilingi 9/lita (sawa na asilimia 0.40) na Shilingi 39/lita (sawa na asilimia 1.83). Aidha, ukilinganisha na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za Petroli na Dizeli zimeongezeka kwa Shilingi 8.84/lita (sawa na asilimia 0.42) wakati bei za jumla za Dizeli zimeongezeka kwa Shilingi 38.74/lita (sawa na asilimia 1.93). Mabadiliko ya bei za mafuta ya Petroli na Dizeli kwa mikoa ya kaskazini yametokana na kuongezeka kwa bei za mafuta katika soko la dunia, mabadiliko ya gharama za usafirishaji wa mafuta (*BPS Premiums*) na kushuka kwa thamani ya Shilingi ya Tanzania dhidi ya dola ya Marekani, fedha inayotumika kununua mafuta. Kutokana na mkoa wa Tanga kuishiwa Mafuta ya Taa, wamiliki wa vituo vya mafuta katika Mikoa ya Kaskazini wanashauriwa kununua mafuta hayo Dar es Salaam na hivyo bei za rejareja za Mafuta ya Taa kwa Mikoa ya Kaskazini zitatokana na gharama za mafuta hayo yaliyopokelewa katika bandari ya Dar es Salaam na kusafirishwa hadi Mikoa ya Kaskazini.
- (c) Mamlaka inapenda kuukumbusha umma kwamba bei kikomo za mafuta kwa eneo husika, zinapatikana pia kupitia simu za kiganjani kwa kupiga namba ***152*00#** na kisha kufuata maelekezo. Huduma hii ni bure na inapatikana kupitia mitandao yote ya simu za mkononi hapa nchini.
- (d) Kwa mujibu wa Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa

taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta. Taarifa hizi zina lengo la kuwasaidia wadau kufanya maamuzi stahiki kuhusu manunuzi ya bidhaa za mafuta.

- (e) **Kampuni za mafuta ziko huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani mradi tu bei hizo zisivuke bei kikomo (*price cap*) kama ilivyokokotolewa na kanuni (*formula*) iliyopitishwa na EWURA na ambayo ilichapishwa katika **Gazeti la Serikali Na. 163/2018 la mwezi April 2018.****
- (f) Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana na yakionesha bei ya mafuta, punguzo, vivutio vya biashara au promosheni zinazotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta katika vituo vinavyouza mafuta kwa bei nafuu zaidi ili kushamirisha ushindani. **Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja. Adhabu kali itatolewa kwa kituo husika kwa kutotekeleza matakwa ya kisheria kwa mujibu wa kanuni husika.**
- (g) Wauzaji wa mafuta ya petroli wanatakiwa kutoa risiti za mauzo kutoka kwenye mashine za EFPP (*Electronic Fiscal Pump Printers*) na Wanunuzi wahakikishe wanapata stakabadhi hizo za malipo zinazoonyesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hizo za malipo zitatumika kama kidhibiti kwa wanunuzi wa mafuta endapo kutajitokeza malalamiko ya aidha kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo au kuuziwa mafuta yasiyo na kiwango cha ubora kinachofaa, na pia, risiti hizo zitasaidia kurahisisha ukusanyaji wa kodi za Serikali zitokanazo na mafuta ya petroli.

A: BEI ZA REJAREJA

Mji	Bei Kikomo		
	Petroli (Shs/Lita)	Dizeli (Shs/Lita)	Mafuta Ya Taa (Shs/Lita)
Dar es Salaam	2,282	2,164	2,192
Arusha	2,291	2,225	2,276
Arumeru (Usa West)	2,291	2,225	2,276
Karatu	2,309	2,243	2,295
Monduli	2,296	2,230	2,282
Monduli-Makuyuni	2,301	2,235	2,286
Ngorongoro (Loliondo)	2,375	2,309	2,368
Kibaha	2,287	2,168	2,197
Bagamoyo	2,294	2,175	2,203
Kisarawe	2,290	2,171	2,199
Mkuranga	2,292	2,173	2,202
Rufiji	2,310	2,191	2,220
Dodoma	2,341	2,222	2,251
Bahi	2,349	2,230	2,258
Chemba	2,368	2,249	2,277
Kondoa	2,374	2,255	2,284
Kongwa	2,339	2,220	2,248
Mpwapwa	2,342	2,224	2,252
Iringa	2,347	2,228	2,256
Kilolo	2,351	2,232	2,261

Mufindi (Mafinga)	2,357	2,238	2,266
Njombe	2,375	2,256	2,284
Njombe (Kidegembye)	2,396	2,277	2,305
Ludewa	2,413	2,294	2,323
Makete	2,406	2,287	2,315
Wanging'ombe (Igwachanya)	2,373	2,254	2,282
Bukoba	2,498	2,379	2,408
Biharamulo	2,472	2,354	2,382
Karagwe (Kayanga)	2,514	2,396	2,424
Kyerwa (Ruberwa)	2,520	2,401	2,430
Muleba	2,498	2,379	2,408
Ngara	2,463	2,345	2,373
Misenyi	2,506	2,388	2,416
Geita	2,448	2,329	2,358
Bukombe	2,437	2,318	2,347
Chato	2,469	2,350	2,379
Mbogwe	2,486	2,367	2,396
Nyang'hwale	2,463	2,344	2,373
Kigoma	2,514	2,395	2,424
Uvinza (Lugufu)	2,526	2,407	2,436
Buhigwe	2,503	2,384	2,413
Kakonko	2,471	2,352	2,381
Kasulu	2,500	2,381	2,410
Kibondo	2,478	2,359	2,388
Moshi	2,280	2,214	2,266
Hai (Bomang'ombe)	2,283	2,217	2,269
Mwanga	2,273	2,207	2,259
Rombo (Mkuu)	2,297	2,231	2,287
Same	2,267	2,200	2,252
Siha (Sanya Juu)	2,287	2,221	2,272
Lindi	2,341	2,223	2,251
Lindi-Mtama	2,359	2,241	2,269
Kilwa Masoko	2,316	2,198	2,226
Liwale	2,362	2,244	2,272
Nachingwea	2,371	2,252	2,280
Ruangwa	2,372	2,253	2,282
Babati	2,325	2,259	2,315
Hanang (Katesh)	2,335	2,269	2,325
Kiteto (Kibaya)	2,340	2,274	2,326
Mbulu	2,337	2,271	2,327
Simanjiro (Orkasumet)	2,357	2,291	2,347
Musoma	2,461	2,342	2,371
Musoma Vijijini (Busekela)	2,502	2,383	2,412
Rorya (Ingirijuu)	2,470	2,351	2,380
Rorya (Shirati)	2,505	2,386	2,414
Bunda	2,452	2,333	2,362
Butiama	2,458	2,339	2,368
Serengeti (Mugumu)	2,507	2,388	2,416

Tarime	2,472	2,353	2,382
Tarime (Kewanja/Nyamongo)	2,477	2,358	2,386
Mbeya	2,390	2,271	2,299
Chunya	2,399	2,280	2,309
Chunya (Makongolosi)	2,413	2,295	2,323
Ileje	2,403	2,284	2,312
Kyela	2,405	2,287	2,315
Mbarali (Rujewa)	2,374	2,255	2,283
Mbozi (Vwawa)	2,399	2,280	2,309
Momba (Chitete)	2,408	2,289	2,318
Rungwe (Tukuyu)	2,399	2,280	2,308
Morogoro	2,307	2,189	2,217
Mikumi	2,323	2,204	2,233
Kilombero (Ifakara)	2,345	2,227	2,255
Kilombero (Mlimba)	2,368	2,249	2,277
Kilombero (Mngeta)	2,357	2,238	2,267
Ulanga (Mahenge)	2,356	2,237	2,266
Malinyi	2,366	2,247	2,276
Kilosa	2,326	2,207	2,236
Gairo	2,326	2,207	2,236
Mvomero (Wami Sokoine)	2,318	2,199	2,228
Turiani	2,333	2,214	2,242
Mtwara	2,355	2,236	2,265
Nanyumbu (Mangaka)	2,404	2,285	2,313
Masaki	2,381	2,262	2,290
Newala	2,387	2,268	2,297
Tandahimba	2,380	2,261	2,290
Mwanza	2,433	2,314	2,342
Kwimba	2,469	2,350	2,379
Magu	2,441	2,322	2,350
Misungwi	2,438	2,319	2,348
Sengerema	2,465	2,346	2,375
Ukerewe	2,492	2,373	2,402
Sumbawanga	2,455	2,337	2,365
Kalambo (Matai)	2,463	2,344	2,372
Nkasi (Namanyeleye)	2,469	2,350	2,379
Katavi (Mpanda)	2,491	2,372	2,400
Mlele (Inyonga)	2,469	2,350	2,379
Mpimbwe (Majimoto)	2,483	2,364	2,392
Songea	2,406	2,287	2,316
Mbinga	2,440	2,321	2,349
Namtumbo	2,435	2,316	2,345
Nyasa (Mbamba Bay)	2,442	2,323	2,352
Tunduru	2,465	2,346	2,375
Shinyanga	2,411	2,293	2,321
Kahama	2,425	2,306	2,335
Kishapu	2,440	2,321	2,350
Simiyu (Bariadi)	2,453	2,334	2,363

Busega (Nyashimo)	2,446	2,327	2,356
Itilima (Lagangabilili)	2,456	2,337	2,366
Maswa	2,444	2,326	2,354
Meatu (Mwanhuzi)	2,451	2,333	2,361
Singida	2,373	2,254	2,283
Iramba	2,385	2,267	2,295
Manyoni	2,358	2,239	2,267
Ikungi	2,369	2,250	2,278
Mkalama (Nduguti)	2,398	2,279	2,307
Tabora	2,437	2,318	2,346
Igunga	2,391	2,272	2,300
Kaliua	2,455	2,336	2,365
Ulyankulu	2,449	2,330	2,359
Nzega	2,401	2,282	2,311
Sikonge	2,449	2,330	2,358
Urambo	2,450	2,331	2,360
Tanga	2,234	2,168	2,238
Handeni	2,255	2,188	2,218
Kilindi	2,270	2,203	2,252
Korogwe	2,246	2,180	2,231
Lushoto	2,255	2,189	2,241
Mkinga (Maramba)	2,241	2,175	2,253
Muheza	2,239	2,173	2,238
Pangani	2,241	2,175	2,245

B: BEI ZA JUMLA

Bei za Jumla – DSM	Petroli (Shs/Lita)	Dizeli (Shs/Lita)	Mafuta ya Taa (Shs/Lita)
Bei Kikomo	2,158.32	2,039.48	2,068.52

Bei za Jumla – TANGA	Petroli (Shs/Lita)	Dizeli (Shs/Lita)	Mafuta ya Taa (Shs/Lita)
Bei Kikomo	2,109.86	2,043.63	1,816.24

Nzinyangwa E. Mchany
KAIMU MKURUGENZI MKUU
EWURA